AfCHPR
Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Wavuti: www.african-court.org
Simu: +255-272-510-510

MUHTASARI WA HUKUMU

PATROKLOS TSAPERAS

DHIDI YA

JAMHURI YA MALAWI

MAOMBI NA. 007/2022

HUKUMU KUHUSU MAMLAKA YA KISHERIA NA UKUBALIFU

TAREHE 13 NOVEMBA 2026

UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU

Arusha, tarehe 13 Novemba 2026: Leo Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) imetoa Uamuzi katika kesi ya *Patroklos Tsaperas dhidi ya Jamhuri ya Malawi*.

Patroklos Tsaperas (Mleta Maombi) ni raia wa Jamhuri ya Afrika Kusini na mkurugenzi wa Malawi Mobile Limited (MML). Alidai kwamba, katika kesi zilizosikilizwa mbele ya mahakama za kitaifa, Jamhuri ya Malawi (Mjibu Maombi) ilikiuka haki yake ya kumiliki mali, haki yake ya kutobaguliwa, haki yake ya ulinzi sawa wa sheria, haki yake ya kutambuliwa kama mtu mbele ya sheria na haki yake ya kesi yake kusikilizwa kwa haki, haki ambazo zinalindwa na Kifungu cha 2, 3, 7(1) na 14 cha Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba), Kifungu cha 17 cha Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu na Vifungu vya 14, 16 na 26 vya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) mtawalia. Pia aliomba Mahakama imlipe fidia.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Itifaki) na Kanuni ya 49(1) ya Kanuni za Mahakama (Kanuni), Mahakama ilianza kwa kuangalia mamlaka yake ya kisheria. Mahakama ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka

binafsi kwa kuwa, tarehe 9 Oktoba 2008, Mjibu Maombi alikuwa Mhusika wa Itifaki na aliwasilisha Azimio lililotolewa chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki hiyo, ambalo linawaruhusu watu binafsi na Mashirika yasiyo ya kiserikali kuwasilisha maombi moja kwa moja mbele ya Mahakama. Mahakama iliamua kuwa ilikuwa na mamlaka ya msingi kwa sababu Mleta Maombi alidai kufanyika ukiukaji wa haki zinazolindwa kwa mujibu wa Mkataba na ICCPR, ambazo Mjibu Maombi ni mhusika.

Kuhusu mamlaka ya kisheria ya muda, Mahakama ilibaini kwamba, ingawa matukio yaliyosababisha mzozo huo yalianza mwaka 2005, kabla ya Mjibu Maombi kuwa mhusika katika Itifaki, madai ya Mleta Maombi pia yalihusu kesi za mahakama za ndani, ambazo zilitokea baada ya tarehe hiyo. Kwa hivyo Mahakama iliamua kuwa ilikuwa na mamlaka ya muda. Hatimaye, ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka ya kieneo, ikizingatiwa kwamba ukiukaji unaodaiwa kufanywa ulitokea ndani ya eneo la Mjibu Maombi. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza Shauri hilo.

Mahakama ilibaini kwamba, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(2) cha Itifaki na Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Mahakama, lazima itoe uamuzi kuhusu ustahiki wa Maombi kwa mujibu wa Kifungu cha 56 cha Mkataba, ambacho masharti yake yanarejelewa katika Kanuni ya 50(2) ya Kanuni za Mahakama. Mjibu Maombi aliweka mapingamizi mawili kuhusu ukubalifu: kwanza, kwamba Mleta Maombi hakuwa amekamilisha taratibu za ndani za kisheria; na pili, kwamba Maombi hayo hayakuwa yamewasilishwa ndani ya muda unaofaa.

Kuhusu pingamizi linalotokana na kutotumia kikamilifu taratibu za ndani za kisheria, Mjibu Maombi alidai kwamba kesi za ndani zilihusu tu ukiukaji wa mkataba na kosa la uchochezi, zaidi ya hayo, hakuna ukiukaji wa haki za binadamu uliodaiwa kufanywa mbele ya mahakama za kitaifa. Mahakama ilichunguza kila madai kivyake. Kuhusu haki ya kumiliki mali, Mahakama ilirejelea kwamba, katika kuamua iwapo kesi iliyofunguliwa na kampuni kunaweza kuhusishwa na mleta maombi mwenyewe, ni lazima kuzingatia uhusiano uliopo kati ya mleta maombi na kampuni. Kuhusiana na jambo hili, Mahakama ilibaini kuwa Mleta Maombi alikuwa ameonyesha uhusiano wa

kutosha na MML kupitia umiliki wake wa hisa kwa njia isiyo ya moja kwa moja na kwamba kesi iliyofunguliwa na MML hadi Mahakama Kuu ya Rufaa ya Malawi (MSCA) ilikuwa imeonyesha kiini cha mzozo huo mbele ya mahakama za kitaifa. Kwa hivyo Mahakama iliamua kwamba Mleta Maombi alikuwa amekamilisha kisheria za ndani kuhusiana na madai yake kuhusu haki ya kumiliki mali.

Hata hivyo, Mahakama ilibaini kwamba Mleta Maombi hakuwa amekamilisha taratibu za ndani za kutafuta haki kuhusiana na madai yake yaliyobaki. Kuhusu madai kwamba MSCA haikuwa na idadi ya kutosha ya majaji ilipotoa hukumu yake, Mahakama ilirejea kwamba haitoshi kwa mleta maombi kutupia lawama ufanisi wa taratibu za ndani za kisheria bila kujaribu kuzitumia zote. Kuhusu ukiukaji unaodaiwa wa haki za usawa mbele ya sheria na ulinzi sawa wa sheria, ambao ulihusiana na madai ya kutotekelezwa kwa hukumu ya kikatiba ya Mahakama Kuu kwa niaba ya Mwenyekiti wa zamani wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano ya Malawi, Mahakama ilibaini kwamba Mleta Maombi hakuwa amefungua kesi zozote za utekelezaji. Kuhusiana na madai yake ya ubaguzi kwa misingi ya utaifa na rangi na haki ya kutambuliwa kama mtu mbele ya sheria, Mahakama pia ilibaini kwamba Mleta Maombi hakutoa ushahidi wowote wa kukamilisha taratibu za ndani za kisheria, wala hakuonyesha kwamba kuna msamaha wowote wa takwa hili uliotumika.

Kwa hivyo, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi kuhusiana na madai ya haki ya kumiliki mali, lakini ikakubaliana kuhusiana na madai mengine.

Kuhusu pingamizi kwamba Maombi hayakuwasilishwa ndani ya muda unaofaa, Mjibu Maombi alidai kwamba Mleta Maombi hakuwa amefungwa gerezani wala hakuwa maskini, alikuwa na uwakilishi wa kisheria unaoendelea na hakuonyesha sababu yoyote ya kuchelewa. Mahakama ilibainisha kwamba kikomo cha muda wa kuzingatiwa kilikuwa kuanzia tarehe 10 Machi 2015, tarehe ya hukumu ya MSCA hadi tarehe 17 Oktoba 2022, yaani, miaka saba, miezi saba na siku saba. Katika uamuzi wake, Mahakama ilibaini kwamba kipindi hiki kilikuwa kirefu zaidi kuliko kile ilichoona kuwa kinakubalika na kwamba, kwa kukosekana kwa sababu yoyote ya msingi, ulikuwa ucheleweshaji usio na msingi na wa kupita kiasi. Kwa hivyo, Mahakama iliunga

mkono pingamizi la Mjibu Maombi na kuona kwamba Maombi haya hayakuwasilishwa ndani ya muda unaofaa, jambo ambalo lilikuwa ukiukaji wa Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni za Mahakama.

Kwa kuwa masharti ya ukubalifu ni ya jumla, Mahakama haikuangalia matakwa yanayosalia na ikatangaza Maombi hayo kuwa hayakubaliki.

Mjibu Maombi aliomba kwamba Mleta Maombi alipe gharama. Katika suala hili, Mahakama ilibainisha kwamba haitozi ada za kuwasilisha maombi na kwamba Mjibu Maombi hakuwa ameonyesha kwamba alikuwa ametumia gharama zozote. Kwa hivyo, iliamuru kila Upande ubebe gharama zake.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 28(7) cha Itifaki na Kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Mahakama, Jaji Suzanne Mengue aliambatisha Maoni Tofauti kwenye Uamuzi huo.

Maelezo zaidi

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, yanaweza kupatikana kwenye tovuti kupitia: https://ajudata.african-court.org/details-case/0072022

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kupitia anwani ifuatayo ya barua pepe: registrar@african-court.org.

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.